/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*No.3* *23rd January, 2024*

***SPECIAL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 3 Vol. 105 Dated 23rd January, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 40B la tarehe 23/1/2024

SHERIA YA TASNIA YA SUKARI,
(SURA YA 251)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 11A)*

AMRI YA BEI ELEKEZI YA SUKARI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Bei Elekezi ya Sukari ya mwaka 2024.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kuanzia tarehe ya kuchapishwa hadi tarehe 30 Juni 2024.

Kiwango cha juu cha bei ya rejareja na jumla

3.-(1) Bei ya rejareja na jumla ya sukari itategemea eneo husika.

(2) Kiwango cha juu cha bei ya mauzo ya sukari katika kila Mkoa kitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

Usimamizi wa bei ya sukari

4. Bodi, kwa kushirikiana na mamlaka husika, itasimamia uzingatiaji wa Amri hii.

Mapitio ya bei elekezi

5. Bei elekezi zilizoainishwa katika Amri hii zitafanyiwa mapitio na Bodi mara kwa mara kadri ya mahitaji.

Makosa

6. Mtu yeyote anayeuza sukari kinyume na bei elekezi zilizoainishwa katika Jedwali atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika masharti ya Sheria ya Tasnia ya Sukari.

Sura ya 251

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 40B (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(2))*

KIWANGO CHA JUU CHA BEI YA SUKARI KWA MAUZO YA JUMLA NA REJAREJA KWA TANZANIA BARA

| NA | KANDA | MIKOA | BEI YA JUMLA (Sh.) | BEI YA REJAREJA (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kwa kilo 1 | Kwa kilo 1 |
| 1. | Nyanda za Juu Kusini | Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe | 2,600 – 2,800 | 2,700 – 3,000 |
| 2. | Kanda ya Mashariki | Morogoro, Dar es Salaam, Pwani | 2,600 – 2,800 | 2,700 – 3,000 |
| 3. | Kanda ya Kati | Dodoma, Singida, Tabora | 2,650 – 2,800 | 2,800 – 3,000 |
| 4. | Kanda ya Kusini | Lindi, Mtwara, Ruvuma | 2,650 – 2,900 | 2,900 – 3,200 |
| 5. | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara | 2,650 – 2,800 | 2,800 – 3,000 |
| 6. | Kanda ya Kaskazini | Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara | 2,600 – 2,800 | 2,700 – 3,000 |
| 7. | Kanda ya Magharibi | Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa | 2,600 – 2,900 | 2,800 – 3,200 |

Dar es Salaam,
23 Januari, 2024

KENNETH M. K. BENGESI,
*Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania*